JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA KILIMO
# BODI YA KOROSHO TANZANIA



# JARIDA LA MWEZI NOVEMBA 2023.

Toleo Jipya

#KilimoBiashara

## 1.0 UTANGULIZI

Soko la zao la korosho duniani limekuwa likipanda na kushuka kulingana na mahitaji na usambazaji. Hata hivyo, uzalishaji wa korosho ghafi umekuwa ukiongezeka duniani na kuongeza ushindani kwa nchi wazalishaji, huku India na Vietnam wakiwa ndio wanunuzi wakubwa wa korosho ghafi zinazozalishwa duniani kote.

Kwa inchi za Afrika hasa hasa Afrika ya Magharibi, Afrika Mashariki (Tanzania) pamoja na kusini (Msumbiji) zinaendelea kukuza na kuimarisha sekta ya korosho kwa kuboresha mfumo wa masoko na pembejeo.



## 2.0. MWENENDO WA SOKO LA KOROSHO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI MWEZI AGOSTI, 2023.

### 2.1. MWENENDO WA SOKO AFRIKA MAGHARIBI

Kwa sasa korosho inayouzwa katika soko la dunia inatoka nchini Tanzania, Msumbiji ambao pia ndio wazalishaji wakubwa kusini mwa ikweta, mauzo nchini Tanzania yalianza tarehe 20 Oktoba, 2023 na mauzo nchini Msumbiji yalianza tarehe 27 Novemba,2023. Kuna kiasi kidogo cha korosho kilichobaki katika msimu uliopita katika nchi za Afrika magharibi ambacho kimeendelea kuuzwa.

### 2.2. HALI YA SOKO LA KOROSHO NCHINI CAMBODIA

Takribani tani 615,000 za korosho ghafi zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 831 zimesafirishwa kwenda Vietnam pungufu ya asilimia kumi na sita (16%) kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Raisi wa CAC (Cashewnut Association of Cambodia) Ndugu Uon Silot alihusisha kupungua kwa mavuno na kushuka kwa bei ya soko la kimataifa na hali mbaya ya hewa iliyosababishwa na mvua kubwa.
Chanzo: African Cashew Alliance

### 2.3. HALI YA SOKO LA KOROSHO NCHINI INDIA

Nchini India masoko ya korosho yameanza taratibu baada ya tamasha la Diwali. Ofa za korosho ghafi kutoka Tanzania zimeshuka kwa takribani Dola za Kimarekani 50 hadi 75 kwa tani. Korosho kutoka Tanzania kwa sasa zinanunuliwa kati ya Dola za Kimarekani 1,250 (CIF) kwa tani hadi 1,280 (CIF) kwa tani ubora wa Ratili 52 (52 lbs) hadi 53 (53 lbs) ambayo inaweza kushuka zaidi katika wiki zijazo.
Chanzo: Cashewnutinformation.



## 2.4. Hali ya Soko la Korosho katika Nchi ya Vietnam


Nchini Vietnam soko la korosho ghafi bado limeendelea kuwa thabiti, kuna mabadiliko kidogo ya bei ya korosho ghafi kulinganisha na mwezi Oktoba. Bei ya korosho ghafi imepanda kidogo kwa mwezi Novemba, bei ni kati ya Dola za kimarekani 1,270 (CIF) kwa tani hadi 1,310 (CIF) kwa tani kwa ubora wa Ratili kati ya 50 (lbs) hadi 53 (lbs) ukilinganisha na mwezi Oktoba ambapo bei ilikuwa ni kati ya Dola za Kimarekani 1,030 kwa tani hadi 1,165 kwa tani ubora wa Ratili 48 (48 lbs) hadi 53 (53 lbs). Mauzo ya nje ya korosho karanga katika nusu ya kwanza Novemba 2023 ni tani 30,066 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 165,726,025 (wastani wa bei ya Dola za Kimarekani 5,512 kwa tani).

**Jedwali Na. 1: Korosho Ghafi Zilizoingia Vietnam Kutoka Nchi Mbalimbali Kuanzia Januari hadi Oktoba, 2023.**

| KOROSHO GHAFI ZILIZOINGIA VIETNAM KUTOKA NCHI MBALIMBALI KUANZIA JANUARI HADI OKTOBA 2023 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| NA | NCHI | KIASI (TANI) | Thamani (CIF) USD | Wastani USD/Tani |
| 1 | Ivory Coast | 783,669 | 851,674,755 | 1,087 |
| 2 | Cambodia | 615,728 | 838,566,545 | 1,362 |
| 3 | Ghana | 236,954 | 255,387,960 | 1,078 |
| 4 | Indonesia | 12,133 | 14,898,348 | 1,228 |
| 5 | Nigeria | 252,134 | 263,439,771 | 1,045 |
| 6 | Tanzania | 98,459 | 132,396,727 | 1,345 |
| 7 | Nyingine | 540,543 | 598,894,920 | 1,108 |
| | **JUMLA KUU** | **2,539,620** | **2,955,259,026** | **1,164** |

**Chanzo:** Cashewnutinformation.

**Korosho Ghafi Zilizoingia Vietnam Kutoka Nchi**



# JEDWALI NA2:BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA NCHI YA INDIA NA VIETNAM JULAI, 2023




**MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI DUNIANI INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI CHA NOVEMBER 2022 HADI Agosti 2023**

| TARAHE | Bei - CIF USD / TON | |
|---|---|---|
| | BEI YA CHINI | BEI YA JUU |
| 14 Januari, 2023 | 1,200 | 1,275 |
| 28 Januari, 2023 | 1,250 | 1,39 |
| 18 Februari, 2023 | 1,180 | 1,230 |
| 13 Machi, 2023 | 1,150 | 1,165 |
| 24 Aprili, 2023 | 1,040 | 1,080 |
| 20 Mei, 2023 | 1,040 | 1,130 |
| 18 Juni, 2023 | 925 | 1,065 |
| 22 Julai, 2023 | 925 | 1,080 |
| 21 Agosti, 2023 | 950 | 1,080 |
| 23 Septemba, 2023 | 1,030 | 1,165 |
| 29 Oktoba, 2023 | 1,100 | 1,285 |
| 19 Novemba, 2023 | 1,270 | 1,280 |
| SOT: 48-53 | | |

Chanzo: Cashewnutinformatio

## JEDWALI NA2:BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA NCHI YA INDIA NA VIETNAM JULAI, 2023




**NB:** Kuanzia Tarehe 14 Novemba, 2023 hadi 19 Novemba, 2023 ni bei ya Korosho Ghafi zinazotoka Tanzania na Ivory Coast.

**Chanzo:** Cashewnutinformation

## 3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji, viwango vya ubora pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

### 3.1 Bei ya Korosho Karanga Vietnam Kufikia Novemba, 2023

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini ikilinganishwa na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Kuna mabadiliko ya bei kwa mwezi Novemba kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3

**Jedwali Na. 3: Bei za Korosho Karanga Nchini Vietnam hadi kufikia Novemba, 2023**

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA Novemba, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAUZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Juu | Bei ya Juu |
| **White Whole Cashews 180** | 180 WW | 8.38 | 8.60 | 20,950.00 | 21,500.00 |
| **White Whole Cashews 210** | WW 210 | 7.72 | 7.94 | 19,300.00 | 19,850.00 |
| **White Whole Cashews 240** | WW240 | 5.73 | 6.17 | 14,325.00 | 15,425.00 |
| **White Whole Cashews 320** | WW320 | 5.18 | 5.51 | 12,950.00 | 13,775.00 |
| **Large Pieces** | LP | 2.76 | 3.64 | 6,900.00 | 9,100.00 |
| **Small Pieces** | SP | 2.43 | 2.65 | 5,790.69 | 6,314.95 |

**Chanzo:** Cashewinformation

### 3.2 Bei ya Korosho Karanga katika nchi za Afrika Magharibi Hadi Kufikia Novemba, 2023

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Novemba, bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni pamoja na Ivory Coast, Ghana na Benin imeshuka kidogo ukilinganisha na mwezi Agosti kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4

**Jedwali Na. 4: Bei ya Korosho Karanga Afrika Magharibi hadi Kufikia Novemba, 2023**

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA NOVEMBA, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | | | | |
| White Whole Cashews 180 | W210 | 7.39 | 7.83 | 18,475.00 | 19,575.00 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 5.95 | 6.28 | 14,875.00 | 15,700.00 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 5.73 | 5.95 | 14,325.00 | 14,875.00 |
| White Whole Cashews 450 | W450 | 5.29 | 5.51 | 13,225.00 | 13,775.00 |
| White Splits | WS | 3.86 | 4.30 | 9,650.00 | 10,750.00 |
| Large Pieces | LP | 3.42 | 3.86 | 8,550.00 | 9,650.00 |
| Small Pieces | SP | 2.65 | 2.98 | 6,625.00 | 7,450.00 |

**Chanzo:** Tanzania Association for Cashewnut Processors **(TACP)**

### 3.3 Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi Hadi Kufikia Novemba, 2023


Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje katika nchi za Uholanzi, Uturuki, Misri, nchi za Uarabuni, Marekani nk. Hakuna mabadiliko ya bei ingawa kutokana na kupanda kwa thamani ya Dola dhidi ya shilingi ya Tanzania kuna mabadiko kwenye bei ya TZS/Kilo kama ilivyo katika jedwali Na. 5

**Jedwali Na. 5: Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi hadi kufikia Novemba, 2023.**

| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA NOVEMBA, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | BEI DOLA/KILO (FOB) | | BEI TZS/KILO (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| WHITE WHOLE CASHEWS 180 | W180 | 8.40 | 9.70 | 21,000.00 | 24,250.00 |
| WHITE WHOLE CASHEWS 240 | W240 | 6.10 | 6.45 | 15,250.00 | 16,125.00 |
| WHITE WHOLE CASHEWS 320 | W320 | 5.75 | 6.25 | 14,375.00 | 15,625.00 |
| WHITE SPLITS | WS | 4.00 | 4.37 | 10,000.00 | 10,925.00 |
| LARGE WHITE PIECES | WS | 4.50 | 4.50 | 10,723.50 | 10,723.50 |

**Chanzo:** Tanzania Association for Cashewnut Processors **(TACP)**

## JEDWALI NAMBA 6: UWIANO WA BEI DARAJA WW320




**Chanzo:** Bodi ya Korosho

### 4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

Mauzo ya korosho ghafi kwa msimu wa 2023/2024 yalianza rasmi tarehe 20 Oktoba, 2023. Hadi kufikia tarehe 29/11/2023 jumla ya tani 214,676,845 za korosho ghafi zimeuzwa kwenye Minada ikilinganishwa na tani 108,957,027 zilizokuwa zimeuzwa katika msimu wa 2022/2023 hadi kufikia kipindi kama hiki kwa njia ya minada. (Rejea jedwali Na. 7a). Malengo ya uzalishaji katika msimu wa 2023/2024 ni kufikia tani 350,000 za korosho ghafi.

Katika Msimu wa 2023/2024 usafirishaji wa korosho ghafi kutoka mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara unafanyika kupitia bandari ya Mtwara, wakati usafirishaji wa korosho za Pwani na Mikoa mingine unafanyika kupitia bandari ya Dar es Salaam na Tanga. Usafirishaji Korosho ghafi kwenda nje ya nchi kupitia bandari ya Mtwara unaendelea ambapo hadi kufikia tarehe 26 Novemba, 2023 jumla ya Makasha matupu 2,650 yenye uwezo wa kufungasha tani 100,954.4 za korosho ghafi yamepokelewa kutoka kampuni mbalimbali za meli (Makasha 172 yenye ukubwa wa futi 20 na Makasha 2,478 yenye ukubwa wa futi 40). Jumla ya Makasha 944 yamepakiwa shehena ya korosho ghafi tani 36,112.54 na kusafirishwa kwenda nchini India, Singapore na Dubai.



## JEDWALI NA. 7A: KOROSHO ZILIZOUZWA KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI.

| Jumla ya Kiasi Kilichouzwa na Thamani (Novemba 21 hadi Novemba 30, 2023) | | |
|---|---|---|
| **KIPINDI CHA** | **KIASI KILICHOUZWA (MT)** | **THAMANI (TZS)** |
| Wiki ya Sasa | 24,746,044 | 42,459,188,921 |
| Jumlishi Wiki iliyopita | 189,930,801 | 459,284,971,451 |
| **JUMLA** | **214,676,845** | **501,744,160,372** |

## JEDWALI NA. 7B: MUHTASARI BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA MINADA

| MUHTASARI BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA MNADA | | | |
|---|---|---|---|
| **WIKI ILIYOPITA (NOVEMBA 14 HADI NOVEMBA 20)** | | **WIKI YA SASA (NOVEMBA 21 HADI NOVEMBA 30)** | |
| **MWENENDO WA BEI** | **Mwezi** | **Daraja la Kawaida** | |
| | | **Bei ya Juu** | **Bei ya Chini** |
| | Bei ya Mwezi Julai | 1,950 | 1,500 |
| | Bei ya Mwezi Juni | 2,035 | 1,700 |
| | Mabadiliko (%) | ▼ **4.2%** | ▼ **11.8%** |

**UFUNGUO** "NA"= Haipo

# JEDWALI NA. 7C: BEI ZA MAUZO YA KOROSHO GHAFI KIMKOA.

| Bei ya Mauzo Korosho Ghafi ya Mkoa (Novemba 21 hadi Novemba 30, 2023) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MKOA | CHAMA KIKUU | WIKI | Daraja la Kawaida | |
| | | | Bei ya Juu | Bei ya Chini |
| MTWARA | MAMCU | Bei ya sasa | 1,855 | 1,700 |
| | | Bei ya Mnada Uliopita | 2,000 | 1,850 |
| | | Mabadiliko (%) | ▼ 7.3% | ▼ 8.1% |
| | TANECU | Bei ya sasa | 1,900 | 1,755 |
| | | Bei ya Mnada Uliopita | 2,035 | 1,902 |
| | | Mabadiliko (%) | ▼ 6.6% | ▼ 7.7% |
| LINDI | RUNALI | Bei ya sasa | 1,950 | 1,750 |
| | | Bei ya Mnada Uliopita | 1,900 | 1,800 |
| | | Mabadiliko (%) | ▲ 2.6% | ▼ 2.8% |
| | LINDI MWAMBAO | Bei ya sasa | 1,701 | 1,500 |
| | | Bei ya Mnada Uliopita | 1,800 | 1,700 |
| | | Mabadiliko (%) | ▼ 5.5% | ▼ 11.8% |
| PWANI | CORECU | Bei ya sasa | 1,820 | 1,800 |
| | | Bei ya Mnada Uliopita | 2,120 | 1,950 |
| | | Mabadiliko (%) | ▼ 14.2% | ▼ 7.7% |
| RUVUMA | TAMCU | Bei ya sasa | 1,618 | 1,605 |
| | | Bei ya Mnada Uliopita | 1,750 | 1,712 |
| | | Mabadiliko (%) | ▼ 7.5% | ▼ 6.3% |

**Chanzo:** Bodi ya Korosho

## 5.0 HALI YA UBORA WA KOROSHO MSIMU WA 2023/2024

Hali ya ubora kwa miaka 3 mfululizo imeendelea kuimarika kwa mujibu wa data za mauzo ya korosho hadi kufikia tarehe 30/11/2023. Korosho daraja kwanza zilizoingia mnadani ni tani 213,867.760 ambazo ni sawa na asilimia 99.623 (99.623%) ya korosho zote zilizouzwa kwa njia ya mnada na korosho daraja la pili ni tani 809.085 ambazo ni sawa na asilimia 0.377 (0.377%) ya korosho zote zilizouzwa mnadani.

Aidha kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na mvua nyingi baadhi ya maeneo kumekuwa na changamoto ya kiwango cha unyevu wa korosho na mkoa wa Pwani baadhi ya maeneo korosho zimekosa sifa za kuingia sokoni sababu ya unyevu mkubwa uliosababisha korosho kuota/kuharibika.

Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa katika kusimamia ubora wa korosho ikiwemo kutoa elimu kupitia redio za kijamii na semina kwa wakulima,viongozi wa AMCOS na maafisa kilimo kata/vijiji, kufanya ukaguzi katika ghala za vyama vya msingi na ghala za mnada na kununua na kusambaza maturubai ya kuanikia korosho katika vyama vya msingi kwaajili ya kuanikia korosho.






# TICC | Tanzania International Cashew Conference 2023

11-13 Oktoba, **2023**

**TANZANIA INTERNATIONAL CASHEW CONFERENCE**


UHURU NA UMOJA
TANZANIA INTERNATIONAL CASHEW CONFERENCE 2023
TANZANIA INTERNATIONAL CASHEW CONFERENCE
GUEST OF HONOR : HON. DR. PHILIP ISDOR MPANGO,
VICE PRESIDENT OF THE UNITED REPUPLIC OF TANZANIA
"INVEST IN CASHEW FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT"

## 6.0 MKUTANO WA KIMATAIFA WA KOROSHO 2023

Mkutano wa kimataifa wa korosho umefanyika tarehe 11-13 Oktoba, 2023 katika ukumbi wa mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere jijini Dar es Salaam. Ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango.
Wazo kuu la mkutano ni "Fursa za uwekezaji kwenye Tasnia ya Korosho Tanzania" na kauli mbiu ni "Wekeza kwenye korosho kwa mendeleo endelevu" (invest in cashew for sustainable development).






Mkutano ulihudhuriwa na wadau wa korosho kutoka nchi 23 ukiwa na zaidi ya washiriki 500 wakiwemo wageni waalikwa, viongozi katika ngazi mbalimbali nchini, mabalozi wa nchi mbalimbali Tanzania, wawasilisha mada(presenters), wawezesha mada (moderator), wachangia mada (panelist), washiriki wa ndani na nje ya nchi.
Mkutano ulifanyika katika ukumbi wa JNICC kwa siku mbili tarehe 11 na 12 na tarehe 13 washiriki 93 walifanya ziara (field visit) katika kiwanda cha AKOFA Mkuranga. Mkutano ulikuwa na mada 12 ambazo ziliwasilishwa na presenter 27, moderator 12 na panelist 54 kutoka ndani na nje ya nchi.


Mada zilizowasilishwa kwenye Mkutano ni pamoja na: Kilimo cha korosho na matumizi ya mashine (Cashew production & Agro-mechanisation); Matumizi ya Teknolojia kwenye Tasnia ya Korosho (Technology transfer in cashew value chain); Fursa za Uwekezaji kwenye Tasnia ya Korosho nchini Tanzania (Investment opportunities in cashew industry in Tanzania); Mfumo wa upatikanaji wa fedha kwenye Tasnia ya Korosho (Financing mechanism in cashew industry);




TANZANIA
THE ROYAL TOUR
TANZANIA
THE ROYAL TOUR
TANZANIA
THE ROYAL TOUR

Teknolojia ya Ubanguaji/Usindikaji wa Korosho (Processing technology and techniques); Matumizi ya soko la korosho na bidhaa zake kwa ujumla (Enhancing marketing of cashew and value-added products globally); Matumizi ya Kidigitali kwenye Tasnia ya Korosho (Digitalization in cashew industry); Motisha na sera wezeshi kwenye Tasnia ya Korosho (Incentives and fiscal policies in cashew Industry) na nyingine.

Lengo la Mkutano lilikuwa ni kutangaza fursa za uwekezaji na biashara katika Tasnia ya korosho na kubadilishana uzoefu na wataalam kutoka nchi mbalimbali. Ambapo kwa kuzingatia kwamba ulikuwa ni mkutano wa kwanza kufanyika nchini, Mkutano huo umefanikiwa kuwakutanisha wadau mbalimbali katika tasnia duniani, umetumika kutangaza fursa katika tasnia ya korosho na kujifunza kutoka mataifa mbalimbali. Mkutano wa kimataifa wa korosho ulifungwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Brigedia Jenerali (mstaafu) Aloyce Mwanjile ndc.




CASHEW FOR

**LIMETOLEWA NA**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
Ni Taasisi Iliyo anzishwa kwa Sheria
Na 18 ya Mwaka 2009.

**MTWARA MAKAO MAKUU**
www.cashew.go.tz

**#Ajenda10/30**